**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti:http://www.utumishi.go.tz

Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
**40404 DODOMA.**

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### MWALIMU WA SEKONDARI KUFUNDISHA MSINGI SIO KUSHUSHWA CHEO

Serikali kuwapangia baadhi ya walimu wa shule za sekondari kufundisha katika shule za msingi ni moja ya hatua katika kuongeza ufanisi na kuleta mgawanyo sawa wa walimu katika shule za sekondari na msingi.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dkt. Laurean Ndumbaro amesema hatua hiyo haimaanishi kuwa walimu wanaotoka katika shule ya sekondari kwenda kufundisha msingi wameshushwa cheo.

Dkt. Ndumbaro ametoa ufafanuzi huo katika kikao kazi na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Makambako. Amesisitiza kuwa lengo la Serikali ni kuondoa upungufu wa walimu katika shule za msingi na kuimarisha utoaji wa elimu.

Dkt. Ndumbaro ameainisha kuwa sifa za kufundisha na kiwango cha elimu zinaendana na mabadiliko yanayotokea duniani, hivyo mwalimu mwenye elimu ya kiwango cha Shahada ya kwanza kufundisha shule ya msingi isionekane ni jambo la ajabu.

Katibu Mkuu Dkt. Ndumbaro amewaambia watumishi wa umma maendeleo katika sekta yoyote, ikiwamo ya elimu yanakuja na mabadiliko hivyo wapokee mabadiliko na kufanya kazi ili kufikia lengo.

**Florence Lawrence**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano

OFISI YA RAIS **(UTUMISHI)**
20 Februari, 2018.